

Nambari ya Mtahiniwa _____

SMZ

BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

MTIHANI WA KURINGILIA KIDATO CHA TATU

021

KISWAHILI

MUDA: SAA 2:30

JUMANNE 28/11/2017 mchana

MAAGIZO KWA WATAHINIWA

1. Mtihani huu una sehemu NNE (4) A, B, C, na D.
2. Jibu maswali YOTE kutoka sehemu A, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu B, maswali MAWILI (2) kutoka sehemu C na swali MOJA (1) kutoka sehemu D.
3. Andika nambari yako ya mtihani katika kila ukurasa.
4. Majibu yote yaandikwe kwenye sehemu zilizoachwa wazi.
5. Simu za mkononi haziruhusiwi ndani ya chumba cha mtihani.

KWA MATUMIZI YA USAHIHISHAJI		
NAMBARI YA SWALI	ALAMA	SAINI
1.		
2.		
3.		
4.		
5.		
6.		
7.		
8.		
9.		
10.		
JUMLA		

Mtihani huu una kurasa 13 zenye maandishi

SEHEMU A: (Alama 20)

UFAHAMU

Jibu maswali YOTE katika sehemu hii

1. Soma habari ifuatayo kwa makini kisha jibu maswali yanayofuata.

Katika hali yetu ya sasa inatubidi tutilie mkazo maendeleo yetu katika vijiji, na hasa katika ukulima. Vile vile inatubidi kwa kadiri ya uwezo wetu, tutumie vifaa vya kisasa zaidi. Lazima tutumie ufundi wa kisasa. Katika sehemu nyingi za nchi yetu tumeanza kufuata ushauri wa mabwana shamba. Lakini chombo chetu kikubwa cha ukulima ni jembe la mkono, na jembe la mkono haliwezi kukidhi haja zetu za kisasa. Hatuna budi kulitelekeza jembe la mkono sasa na tutumie jembe la ng'ombe au plau.

Hatuwezi kuwa na maendeleo kwa kungoja mpaka mkulima apate uwezo wa kununua trekta, aweze kuliendesha na kulitunza. Kwa kweli tukisubiri wakati huo, hatutaweza kamwe kuliacha jembe la mkono maana njia za ukulima zitumikazo sasa haziwezi kuleta uchumi katika nchi utakaotuwezesha kununua matrekta ya kutosha nchi nzima. Pia hatuwezi kuwafundisha watu kuyaendesha na kuyatunza matrekta hayo. Kwa wakati huu matrekta hatuyamudu, hatuna fedha wala mafundi lakini tutayari kabisa kutumia plau la kukokotwa na ngo'mbe. Wanyama tunao na maplau yanaweza kununuliwa kwa bei ndogo na hata kutengenezwa humu nchini.

Plau ni chombo kisichotaka ujuzi mwingi ambacho hata wakulima wetu wanaweza kujifunza kwa wepesi sana na kukitumia. Vile vile ni chombo kinachofaa kukitumia katika mashamba ya umoja ya vijiji vya ujamaa tunavyotarajia kuvijenga, au hata katika shamba la kutosha ambalo mkulima mwenye juhudi na jamaa wanamudu kulilima.

Kwa hivyo, hatuna budi kubadili hali hii kwa kutumia kwa juhudi yote vifaa tunavyomudu kuvitumia au kuvitengeneza. Vifaa ambavyo ni rahisi mkulima kuvitumia bila ya matata au kuharibika, vifaa ambavyo vinafanana na mipango yetu ya sasa na ya miaka michache ijayo. Na hivyo tunaweza kufanya plau la ng'ombe, gari la ng'ombe, kutumikisha punda wetu ambao mpaka sasa wanakula majani yetu bila ya kufanya kazi yoyote. Mambo haya yanaweza kutuongezea sana mazao na kuinua maisha yetu.

Maswali:

a) Andika kichwa cha habari uliyoisoma.

b) Kwa nini hatuwezi kuwa na maendeleo kwa kungoja mpaka mkulima apate uwezo wa kununua trekta?

c) Taja vifaa ambavyo tunaweza kuvitumia kwa sasa ili kuinua maisha yetu.

d) Kwa nini mwandishi ameshauri tutumie vifaa vinavyofanana na mipango yetu ya sasa na miaka michache ijayo?

e) Andika maana ya maneno yaliyopigiwa mstari.

2. Fupisha habari uliyoisoma kwa maneno yasiyozidi ishirini na tano (25).

SEHEMU B: (Alama 30)

SARUFI NA MATUMIZI YA LUGHA

Jibu maswali MAWILI (2) tu katika sehemu hii. Swali la TANO (5) ni la lazima.

3. a) Kwa kutumia mifano elezea kwa ufupi tofauti ya kitenzi shirikishi na kitenzi kisaidizi.

b) Tunga sentensi kwa kutumia vipashio vifuatavyo:

i) W + V + Ts + T + E + E

ii) H + E + t + N + V

c) Ainisha viwakilishi vilivyopigiwa mstari katika sentensi zifuatazo:

i) Mwenyewe amefika mapema.

ii) Wale wataandikisha baadae.

d) Onesha mzizi katika maneno yafuatayo:

i. Kikapu

ii. Wanakimbizana

e) Kwa kutoa mifano miwili (2) ya maneno, elezea kwa ufupi maana ya kutohoa.

4. a) Zichunguze mofimu zilizopigiwa mstari na ueleze hali mbali mbali zinazooneshwa na mofimu hizo.

i) Anatambaa

ii) Hukimbia

iii) Amenikera

iv) Wakinipamba

- b) Unda maneno manne (4) yanayotokana na shina “pika”.

- c) Ainisha maneno yaliyotumika katika sentensi zifuatazo:

i) Polepole! Utatumbukia shimoni.

ii) Aliingia ukumbini polepole.

- d) Toa mfano mmoja mmoja kwa kila aina za maneno yafuatayo:

i) Viingizi

ii) Kitenzi kikuu

- e) Onesha viambishi tamati vyote katika neno lifuatalo na ueleze dhima za viambishi hivyo.

-Wanapikiana

5. a) Eleza maana mbili (2) za sentensi zifuatazo:

- i) Ukija njoo na nyanya.

- ii) Nambari yenyewe ni saba saba tatu.

- b) Fafanua sifa mbili (2) za misimu.

- c) Elezea kwa ufupi jinsi matumizi ya lugha yanavyotegemea mambo yafuatayo:

- i) Uhusiano wa wazungumzaji

- ii) Mukstadha

Nambari ya Mtahiniwa _____

- d) Andika mifano ya mitindo ifuatayo ya lugha.

- i) Hotelini

- ii) Sokoni

- e) Tofautisha kati ya Kamusi la Kitaaluma na Kamusi la Semi.

SEHEMU C: (Alama 30)

FASIHI

Jibu maswali MAWILI (2) katika sehemu hii. Swali la SITA (6) ni la lazima

6. Tunga igizo fupi linalohusu "Athari za Ugonjwa wa Ukimwi".

This image shows a single sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

Nambari ya Mtahiniwa _____


a) Eleza kwa ufupi kwa nini fasihi simulizi inaambiwa ni hai.

b) Eleza maana ya methali zifuatazo:

i) Mwenda tezi na omo hurejea ngamani.

ii) Mchumia juani hulia kivulini.

c) Kamilisha mchoro ufuatao kwa kutaja vipera vinne (4) vya semi.



d) Toa tofauti kati ya utenzi na ngonjera.

e) Taja vipengele vinne (4) vya kuzingatia unapohakiki fani ya kazi ya fasihi simulizi.

8. a) Elezea kwa ufupi maana ya istilahi zifuatazo:

i) Dhamira

ii) Ujumbe

b) Unadhani kuna umuhimu gani wa kuhifadhi kazi za fasihi simulizi? (Taja vipengele viwili (2) tu vya umuhimu huo).

c) Toa methali moja ambayo ungeweza kutumia “kuonya” au “kuadilisha” kulingana na tukio lililoelezwa hapo chini.

i) Mtoto alilelewa vibaya na hatimae akawa jambazi.

Methali: _____

ii) Ndege alijenga kiota kwa kuchukua jani moja moja na hatimae baada ya siku tatu kiota kilikamilika kujengwa.

Methali: _____

d) Eleza kwa ufupi maana ya vipera vifuatavyo vya maigizo.

i) Vichekesho

ii) Majigambo

e) Lete maana ya nahau zifuatazo:

i) Amekula kalenda

ii) Ameasi ukapera

Nambari ya Mtahiniwa _____

SEHEMU D: (Alama 20)

UANDISHI

Jibu swali MOJA (1) katika sehemu hii

9. Chagua tatizo (kero) linaloikabili jamii yako iliyokuzunguka na uliandikie dayalojia. (maneno 120 - 130).

AU

Tunga Insha ya maneno yasiyopungua 120 na yasiyozidi 130 kwa mada ifuatayo:
"Kukosea njia ndio kujua njia"

This image shows a single sheet of white paper with horizontal ruling lines. The lines are evenly spaced and run across the width of the page. There are no margins, text, or other markings on the paper.

10. a) Taja mambo manne (4) muhimu ya kuzingatia wakati wa kuandaa matangazo ya bidhaa au huduma kwa jamii.

- b) Andaa kadi ya mwaliko wa chai ya harusi itayofanyika mwezi ujao.

Nambari ya Mtahiniwa _____
